**TEGA SIKIO UJIFUNZE: EPISODE 9**

**" Ni kwanini (Magurudumu) Tairi za gari ni Nyeusi"**

Mwandishi: Lydian Heller
Mwelekezi : Maja Dreyer
Tafsiri : Anne Thomas/Eric Ponda

**Wahusika**

| | |
|---|---|
| Mtangazaji | |
| Jenny | (14) |
| Jack | (15) |
| Miriam Rafikiye Jenny | (14) |
| Tom Kakake Jack | (18) |

**SEHEMU**
Karakana
Chumbani (nyumbani kwa kina Mariam)

**Sauti**

*Sauti ya redio ikitoweka taratibu*
*Vyuma vikikwaruzana*
*Kisanduku cha vifaa vya karakana kikifungwa kwa fujo*
*Skurubu ikikazwa na spana*
*Chuma kikisuguliwa haraka haraka,kisha polepole,na kukatizwa ghfla*
*Hatua zikikaribia*
*Mfuko ukiangusha chini*
*Hatua zikikaribia.. za Mtu mmoja, kisha wawili*
*Funguo na safaru zikikwaruzana.*
*daftari yanguka na kutawanyika*
*Makaratasi yakitawanyika*
*Injini ya gari ikinguruma*
*Gari likikanyagwa mafuta*
*" " likizimwa*
*Soda ikifunguliwa,yafurika kutoa povu na kumwagika*
*Mtu akinywa soda, na kutoa pumzi ya kuburdika*
*Chupa ya soda ikiwekwa mezani*
*Mchakacho wa mfuko wa plastiki*
*Mtu akichakura chakua vyuma*

**INTRO**

**(Mtangazaji)**

**Karibu tena mpenzi msilizaji wa kipindi hiki cha kuelimisha 'Tega sikio ujifunze'. Ni kipindi kinachotufunza mengi tu kuhusu matukio ya kila siku ambayo huchukuliwa kuwa ya kawaida pasi na kufahamu jinsi yanavyotendeka.Hivi leo Jack amezua mjadala kwanini magurudumu ya Gari ni meusi. Kakake Tom, ambaye ni makanika wa magari, wanajaribu kulifufua gari kuu kuu, na Jack anataka magurudumu ya gari hilo pia yapakwe rangi za kupendeza. Lakini Tom anamuona mpumbavu huku Jenny akiwa amekasirishwa na hatua ya Jack ya kumpuuza na kuzingatia zaidi masuala ya Magari.**

*(Jack na Tom wanang'ang'a kulifufua gari kuu kuu huku wakipeana magizo')*

*(Sauti ya redio ikitoweka taratibu, Vyuma vikikwaruzana, Kisanduku cha vifaa vya karakana kikifungwa kwa fujo, skurubu ikikazwa na spana)*

**Tom: Hebu shikilia hii kidogo?**

**Jack: "Sawa! *(akiguma huku akiunua kitu kizito)***

**Tom: Hapo ni sawa!, sasa nipe spana namba tano *(akichakura sanduku la spana na kukaza nati)***

**Jack*:(akiwa na shaka)* Unadhani mabati haya yatarudi tena barabarani**

**Tom: Kwanini yasirudi, utaliona tena barabarini, *(akirusha chini chuma)*,Lakini ni lazima tuteremshe injini kwanza *(akichakura chakura vyuma vilivyojaa kutu)***

**Jack:** Pia tunahitaji tairi mpya, --hizi zimekwisha kabisa!
*(akinoa chuma)*

*(hatua zikikaribia….(Jenny awasili)*

**Tom :** (*akipiga mbinja za kubabaika kwa kumuona  mwanamke)*
Habari yako Jenny! **Ahha, kupusa katembelea karakana hii yetu chafu!**

**Jenny:** ***(akiwa amekasirika,lakini abadili mbinu)*** **Habari Tom, kwa kweli nilikuwa nikimtafuta Jack… yupo?**

**Jack** *(kwa juhudi,ajivuta nje kutoka chini ya gari)*
Naam niko hapa!, nilikuwa chini ya gari kuchunguza chunguza hali *(akigeuza geuza)* ilivyo… Habari Jenny!"

**Jenny:** *(akifurahia huku akitaka kujua zaidi kuhusu kazi hiyo)*Njema! Unajisikia kama…..

**Jack:** *(akimpuza na kumgeukia Tom)*  Ehh huko chini ya gari kumeoza, bomba lote la ekzosi limeshika kutu.

**Tom:** "Labda Joseph ana akiba nitamuliza ---- yeye ni rafiki yangu sana"

**Jenny:** *(akijaribu kumzungumzia lakini hana uhakika)* ..Jack?

**Jack:** *(kana kwamba ndio mwanzo anamuona)* Vipi Jenny!
…waendeleaje?

**Jenny***:(audhikan na tabia ya Jack ya kumpuuza)* "Nilitaka kujua iwapo unajisikia kama…."
Jack *(akiendelea kuzungumza na Tom)* "Ni wapi tunaweza kupata tairi mpya Tom?"

**Jack:** *(kwa msisimko)* Waonaje hizi tairi tukizipaka utepe wa rangi inayofanana na gari lenyewe ?"

**Tom:** subutu!.. Sitakubali gari lenye rangi nyingi zisizo na maana. isitoshe huwezi kupata tairi zenye rangi,…zote ni nyeusi**!**

**Jack:** *(haamini, huku akiwa amevunjika moyo)* Kwani, si Jenny alikuwa hapa sasa hivi?

***MUZIKI…***…

**<u>Scene 2</u>**

*(Mfuko yarushwa chini/ Funguo na sarafu zikwaruzana, jarida laanguka)*

**Jenny:** *(kwa sauti ya hasira tayari amekasirika kwa muda)*
Sasa waona niliyokwambia Mariam?, **SIAMINI**!!!. Kwani yeye ni nani?, nakwambia sitakubali……"

*(majarida na makaratasi yakirudishwa kwenye mkoba)*

**Mariam:(***akiwa ametishika, na kuuliza kwa hofu)* Jenny? kabla huja kigeuza chumba changu kuwa uwanja wa vita nieleze kinachokukasirisha?

**Jenny**: (kimya kidogo) Hakuzngumza! *(akipumua kwa hasira),* Unajua nilikwenda kumuona Jack ili twende kunywa soda mahali..”

**Mariam:** *(akimhurumia)* akakataa?”

**Jenny:(***akizidi kuudhika),* Hata, hakusema CHOCHOTE, aliniacha nizungumze peke yangu kama mwenda wazimu,… hakushughulika hata kunisikiza, *(akivuta pumzi tena hasira),* hata sidhani alikuwa na habari niko mahali hapo..”

**Marima*:(****akiwa amechanganyikiwa)* Kweli!.. lakini hiyo si tabia yake, *(kwa huzuni)* kila mtu anajua Jack anakupenda  sana!”

**Jenny:** *(bado ameudhika)* Ni kweli *(aking’ata meno)* Inaonekana anashughuli muhimu zaidi kuliko mimi,… ya kufufua mkebe wa gari,.. yeye ya kakake Tom!.  Hawataki kuona wasichana kama mimi mahali hapo!.

**Mariam:** *(akiwaza)*  hmm….nashangaa

**Jenny:** *(bado amekasirika )*Unashangazwa na nini!. Ungewasikia wakizungumza ,kana kwamba kuna siri  kwa sababu ya mkebe huo! *(akiwaiga)*… nipe spana nambari tano!….hili difrensha limejaa kutu!… sijui hili na lile..! sasa mimi ningefanya nini?

**Mariam: Nashangaa tu iwapo  ungeweza kuwasaidia. Labda ungejifunza maana ya maneno hayo. Na hakika ungemfuahisha Jack. Kwanini usijaribu? Pengine kuna mambo ambayo hawayajui!**

**Jenny : Hmmm (*afurahi kidogo)….* Jack alitaka gari liwekwe tairi za rangi lakini Tom anasema hilo haliwezekani ni jambo la upuzi,kwani tairi kawaida huwa ni nyeusi . Japo….."**

**Mariam:** ***(akimpa moyo)*** **"Hebu twende kuliulizia jambo hili"**

**Jenny:** "Gani?"

**Mariam:** Kama kuna tairi za rangi, na kama hakuna ni kwanini *(akimuamuru)* twende!"

***Muziki...***

**<u>SCENE 3</u>**

*Katika  Gareji*

*(Injinin ya Gari ikinguruma)*

**Tom**: *(Sauti yake yamezwa na mngurumo wa Injini)* …Izime!

*(mafuta yakikanyagwa na mngurumo wazidii)*

**Tom:*(****akiwa ameshtuka)* Si mafuta mengi hivyo wewe mjinge!

*(mngurumo wapungua)*

**Tom:***(kwa ukulele)* Sasa jaribu Klachi!…KLACHI!

*(Injini yazimwa)*

**Jack:** *(amechanganyikiwa)* Bado inanguruma vizuri, hebu tupumzike sasa.."

*(Chupa ya soda yafunguliwa, povu latoka na kumwagika. Watu wakinywa soda na kutoa pumzi ya kuburudika)*

**Jack** *(kwa uchovu)*Tumekuwa tukifanya kazi kwa bidii, lakini nadhani mambo yatakuwa mazuri zaidi wakati gari litakapoingia barabarani. Tutakuwa…. *( akipiga tama la soda)….* .Na je kuhusu tairi?

**Tom:** *(akiwaza)* Bado *(pia akipiga tama la soda)* Joseph hana hizo tairi

*(Hatua zikikaribia)*

**Jenny:** *(akikaribia, akijihisi mshindi nakwa uhakika*) Gari hili la **Volkswagen 1200 Beetle linahitaji rimu za ukubwa wa inchi 15 na tairi za ukubwa 5.6 na nchini 15, iwapo unataka kuhifadhi muundo wake. Lakini ni ghali mno hizo na hazipatikani….. Vipi jamaa!**

**Jack:** ***(kwa mshangao)***Habari Jenny!... eeh umesemaje?

**Tom:** *(pia akiwa ameshangaa, huku akimtaza Jenny kwa udadisi) (akijigamba kwa Jack)* Hasa hizo ndizo tairi tunazotaka sijui tutazipata wapi! Kwa hivyo wewe Jenny ni mtaalam wa magari!

**Jenny;** *(akihisi mshindi,ingawa anajisikia kupakwa mafuta na mgongo wa chupa)* Hmmm.. najua wauazji wachache wa tairi wa reja reja ambao wanafahamikiana na watengenezaji. Na mimi huwauliza maswali kuhusu tairi!.

**Jack** ***(****akisikia wivu)* Oooh lakini tulitaka kujua iwapo kunazo aina hiyo ya tairi unazotaja ikiwa zina rangi!.

**Tom:** *(akimkatiza)* Unataka kujua hivyo Jack! *(akijipendekeza kwa Jenny)* mimi najua tairi zote za magari ni nyeusi, au sivyo Jenny?"

**Jenny:** *(akijihisi mwerevu zaidi)* Ni kweli, Tairi nyingi za magari ni nyeusi, kwa sababu hutengenezwa na raba. Raba huwa nyororo na yenye mgando kama chingamu, na huwa ya rangi hudhurungi nyepesi, ambayo haiwezi kutumika ikiwa hivyo. Lakini ikichanganywa na Kaboni, tairi huwa ngumu na ndio sababu haziwezi kuganda barabarani. Kaboni huwa nyeusi na ndio sababu huzifanya tairi kuwa nyeusi!.

**Tom:** ***(akijisikia bora zaidi)*** Hasa, si nimesema mimi,….tairi za rangi ni upuzi mtupu!. Sasa wacha nikendelee na kazi yangu*…"(akinoa chuma)*

**Jenny:** *(akimjuza zaidi)* Hebu kidongo!. Watengenezaji wengi wa magari hawatumii tena Kaboni kwa tairi,.. wanatumia Silika,..mchanganyiko wa kemikali ambao ni bora zaidi kuliko Kaboni kutokana na uwezo wake wa kushikanama haraka na thabiti. Tairi zinazotengenezwa na mchanganyiko huu wa Silika, huvutika kwa urahisi na kunata na ushika vizuri barabarani!. Mchanganyiko huu wa Silika huwa mweupe na hivyo watengenezaji tairi wanaweza kuchanganya na rangi watakazo… wakipenda!

**Jack:** *(akivutiwa na habar hizo)* Inamana… *(akiweka glasi mezani)*, unamaana kwamba ziko tairi za nagi?

**Jenny:** *(akifurahi)* Kunako miaka ya 90, kampuni ya Michelin ilijaribu kutengeneza tairi za rangi ya kijani na samawati, lakini *(akicheka)* kwa sababu ya ukosefu wa wateja wakaacha.Hakuna mtu alitaka kununua kabisa ndiposa wakarudia kutengeneza hizi nyeusi!

**Tom:** *(akijigamba huku akinoa chuma)* Hayo ndiyo niliyokuwa nikisema tangu mwanzoni!…. Ni upuzi na wateja hawataki!

**Jenny***: (akicheka)* Isipokuwa viongozi a magenge nchini Marekani….kuna hadithi.. (akicheka) miaka michache iliyopita kampuni hiyo ya Micheline pia ilifanya majaribio ya kutengeneza tairi za utepe mweupe ubavuni---rangi nyekundu,njano na samawati.. na kadhalika. Lakini wanunuzi walikuwa hao hao viongozi wa magenge kutoka Los Angeles, ili kujitambulisha na magenge yao. Hata hivyo tairi hizo ziliondolewa kwenye soko. *(akicheka tena)*

**Tom:** *(akikatiza shughuli yake ya kunuo chuma na kuzungumza peke yake)*"Viongozi wa magenge tajiri nchini Marekani?"

**Jenny**: *(acheka)* Kweli yashangaa!

**Tom:** Jack, labda tunaweza kununua tairi zenye utepe mwekundu ubavuni sawia na rangi ya gari.

**Jack:** Wacha wee, Sitaki kuonekana mjinga!

**Tom:** *(Akijaribu kuwa mnyenyekevu)* Kwanini? Unajua waweza kuwa Boss wa genge hili!.

**Jack:** *(kwa hasira)* ..Subutu!!

**Jenny:** *(akiwakatiza wote)* Nyamazeni sasa..! *(akijifanya kuwahurumia)* Nilijua sitaweza kuwasaidia kuwasaidia na utafiti wangu *(kwa utundu na kejeli)* lakini pia ni ngependa kuona huu mkebe wenu ukibadilika na kuwa gari la kifahari mnaloweza kujivunia nyinyi wawili, na ndiyo sababu nimewaletea zawadi hii kwenye mfuko!

*mchakacho wa mfuko wa plastiki*

**Jenny:** *(akitaharuki)* fungueni muone, nilifikiria kumshonea hizi..(kimya kidogo)..

*(hatua zikikaribia)*
*mchakacho wa mfuko wa Plastiki*
*mikono ikichakura*
***Mikono ikichakura***

**Jenny:** *(akiwa amefurahi )*Ha haaaaah ni nzuri kweli!.

**Tom:** *(akivunjika moyo)* Foronya za viti. Oooooh Mungu wangu!

**Tom na Jack:(***wakishtuka,na kuchanganyikiwa)* Tena za rangi ya waridi!

**OUTRO**
**Mtangazaji.**

**Kama tulivyosikio maswali mengi tu kuhusu Tairi za magari,mchanganyiko wa kemikali za kutengenezea gtairi,na magenge---- Ni baadhi tu ya maada zinazozua maswali mengi maishani ambayo mara nyigi hupuuzwa au kuchukuliwa mambo ya kawaida. Asanetni kwa kutusikiliza. Ni Mchezo ulioandikwa na Lydia Heller na bila shaka utakuwa na wakati mzuri na kufurahia utafiti wako. Iwapo ungependa kusikiliza tena makala haya, unaweza kufanya hivyo kupitia mtandao wetu www.dw.de/kiswahili. Hadi wakati mwengine…..**

**…Kwa heri.**